Jinsi bima ya mifugo inavyofanya kazi

Mifugo ni pamoja na ng'ombe wa maziwa, ndege wa kufugwa, kondoo, mbuzi, nguruwe na farasi, miongoni mwa wengine. Bima ya mifugo hutolewa kwa majanga kama vile magonjwa ya wanyama. Wakati mwingine, mkulima anaweza kulazimika kuchinja wanyama kwa misingi ya kiafya au kwa ushauri kutoka kwa daktari mtaalamu wa mifugo. Matatizo mengine ni pamoja na wizi, moto na kupigwa na radi. Bima inaweza kujumuisha vilevile kupotea kwa mifugo hao wanapokuwa wakisafirishwa.

Bima ya kilimo na mikopo kwa wakulima

Katika visa vingi, wakulima huhitaji mikopo kutoka taasisi za kifedha kununua vifaa vya kutumia shambani kama vile mbegu, mbolea na kemikali miongoni mwa vingine. Wakulima vilevile huhitaji pesa kununua kemikali, dawa, vifaa vya ujenzi na kadhalika. Hata hivyo, taasisi za kifedha, haziwapi wakulima mikopo kwa urahisi bila udhamini. Wakiwa na bima, taasisi za kifedha hupata hakikisho kwamba mikopo hiyo italipiwa kukipatikana hasara mashambani. Mipangilio inaweza kufanywa ili malipo kwa hasara inayopatikana kutoka kwa bima ilipie mikopo waliyochukua wakulima kutoka kwa taasisi hizo za kifedha moja kwa moja.

Basi sasa nenda ukanunue bima ya mimea na mifugo ili ujihakikishie utulivu na amani wakati unapokuwa mgumu kwako.

> **"Mifugo ni pamoja na ng'ombe wa maziwa, ndege wa kufugwa, kondoo, mbuzi, nguruwe na farasi, miongoni mwa wengine.**

Insurance Regulatory Authority
Bima Bora kwa Taifa
IRA

IRAKenyaPage @ira_kenya

www.ira.go.ke

Insurance Regulatory Authority
Zep-Re Place, 7th Floor
Upper Hill, Longonot Road, off Kilimanjaro Avenue

P.O. Box 43505 GPO 00100, Nairobi Kenya
Tel: +254-20-4996000
Mobile: +254 - 719 047000
Email:commins@ira.go.ke

Help Desk
Toll-free Line: +254 - 0800724499
Email: customercare@ira.go.ke
complaints@ira.go.ke
ethics@ira.go.ke

Insurance Fraud Investigation Unit
Hotline: +254 - 707598455, +254 - 786595455
Email: ifiu@ira.go.ke

Policyholders Compensation Fund
Tel: +254-20-4996238
Email: info@pcf.co.ke

Insurance Regulatory Authority
Bima Bora kwa Taifa
IRA

BIMA YA **MIMEA NA MIFUGO**



BIMA YA **MIMEA NA MIFUGO**

Kilimo na uchumi

Kilimo cha mimea na ufugaji ni uti wa mgongo wa uchumi wa Kenya. Kilimo cha mazao na ufugaji kwa pamoja huipa Kenya mapato mengi kutokana na mauzo katika nchi za nje. Sekta hii ni muhimu katika kuihakikisha nchi ina chakula cha kutosha. Sekta hizi mbili huchangia 22% ya Uchumi wa Kenya (GDP).

Matatizo yanayowakabili wakulima nchini Kenya

Kilimo cha mazao na ufugaji nchini Kenya kinakabiliwa na changamoto nyingi. Hali hii inafanya ngumu kwa wakulima wa Kenya kupata mazao ya kuridhisha. Matatizo kama vile haja ya kupanda mbegu zinazofaa kwa wakati unaofaa na mahali panapofaa na kutumia mbolea inayofaa yanaweza kushughulikiwa kupitia kwa kilimo bora cha mimea na ufugaji. Hata hivyo, changamoto nyingine kama vile mabadiliko ya hali ya hewa, mvua nyingi na kiangazi, mitetemeko ya ardhi, magonjwa, uharibifu, wadudu na mengine ni mambo ambayo mkulima hana uwezo juu yake.

Sekta hizi mbili huchangia asilimia

22% ya Uchumi wa Kenya (GDP)

Insurance Regulatory Authority
IRA
Bima Bora kwa Taifa

Protecting the crops and livestock you treasure against unforseen calamities

#YourSafetyComesFirst

Bima ya mazao ya mimea na mifugo huwalipa wakulima kwa hasara dhidi ya mabadiliko katika mifugo na mazao ya mimea kutokana na hatari zilizotajwa hapo juu. Hii ni njia ya hakika ya kumfanya mkulima awe na ukakamavu kuimarisha shughuli zake baadaye.

Kwa nini uchukue bima ya mimea na mifugo?

Bima ya mifugo ni bima ya wanyama wa kufugwa kama vile ng'ombe, ndege (kuku, bata, batamzinga na kadhalika), kondoo, mbuzi, nguruwe, farasi na kadhalika. Wanyama hawa wanaweza kuathiriwa au kufa kutokana na kiangazi, magonjwa, ajali na misiba kama vile kuzuka kwa maradhi, wizi, moto, kupigwa na radi, kimbuga na mafuriko. Kwa upande mwingine, bima ya mazao ya mimea hushughulikia mazao ya vyakula kama vile ngano, shayiri, miwa, mahindi, mchele na kadhalika. Bima ya mazao ya mimea na mifugo huwalipa wakulima kwa hasara dhidi ya mabadiliko katika mifugo na mazao ya mimea kutokana na hatari zilizotajwa hapo juu. Hii ni njia ya hakika ya kumfanya mkulima awe na ukakamavu kuimarisha shughuli zake baadaye.

Jinsi bima ya mimea inavyofanya kazi

1. Kampuni ya kutoa bima hukubaliana na mkulima kuhusu mazao yanayotarajiwa kwa kila ekari inayochukuliwa bima. Kiasi cha kuwekwa kwenye bima kitategemea jumla ya mazao katika eneo husika. Ikiwa wakati wa kuvuna mkulima anapata chini ya mazao yaliyotarajiwa katika makubaliano, kampuni ya bima inalipia tofauti itakayopatikana hapo. Hivi, mkulima anahakikishiwa mavuno yake aliyotarajia licha ya kutofanikiwa kwa mimea;

2. Mpango mwingine ni pale ambapo kampuni ya bima inamlinda mkulima dhidi ya hasara yoyote inayoweza kutukia kutokana na majanga kama vile ukame, mafuriko, magonjwa, moto na kadhalika. Mkulima anapaswa kupiga ripoti ya uharibifu kama huo kwa kampuni ya bima. Kampuni hiyo itakagua kiwango cha hasara na kupanga malipo ya kiasi cha hasara iliyopatikana kutokana na uharibifu huo.